

USIMAMIZI WA PAMOJA WA MAENEO YETU YA UVUVI UTAIMARISHA UVUVI ENDELEVU KWENYE JAMII ZETU

MAANA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA PAMOJA WA MAENEO YA UVUVI

Shehia/vijiji zaidi ya viwili
vinakubaliana kusimamia kwa
pamoja maeneo yao ya uvuvi ili
kukabiliana na changamoto
zilizopo na kuboresha
usimamizi
endelevu

FAIDA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA PAMOJA WA MAENEO YA UVUVI

- Kupunguza gharama
- Kudhibiti muhali
- Kuwa na haki ya kutumia vifaa vya usimamizi wa kwa kila mmoja kama vile boti
- Kurahisisha kuwakamata wahalifu na kupunguza uvuvi haramu
- Kuwa na mipango na taratibu za uendeshaji zinazolingana
- Ustawi wa rasilimali za bahari
- Ustawi wa mashirikiano ya kijamii

HATUA ZINAZOPITIWA KATIKA KUANZISHA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA PAMOJA WA MAENEO YA UVUVI

- Kutafuta idhini na makubaliano kutoka Idara ya maendeleo ya Uvuvi na Halmashauri ya Wilaya
- Kujenga uelewa jamii kuhusiana na usimamizi wa pamoja kupitia mikutano mbali mbali ya Shehia
- Kukubaliana kwa Shehia au vijiji husika kupitia kamati za uvuvi za Shehia au vijiji husika
- Kuunda kamati itakayoratibu usimamizi wa pamoja wa eneo
- Kuandaa mpango wa pamoja wa usimamizi wa maeneo husika
- Kuandaa ramani ya maeneo
- Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa maeneo ya pamoja
- Kujenga uelewa wa wanajamii kuhusiana na makubaliano yaliyofikiwa
- Kufanya doria za pamoja
- Kuunganisha sheria ndogo ndogo za usimamizi wa pamoja

KAMATI YA URATIBU YA ENEO LA USIMAMIZI WA PAMOJA:

Inaundwa na wajumbe kutoka Kamati za Uvuvi, Masheha wa shehia zilizokubaliana, Afisa Uvuvi Wilaya na Diwani wa eneo husika inafanya kazi kuratibu utekelezaji wa shughuli za pamoja.